JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

**SHULE YA SEKONDARI SAME**
**S.L.P. 17,**
**SAME.**
**TAREHE: 01 /04/2022.**

*SHULE YA SEKONDARI SAME*
*SIMU.*
*SHULE:* ***0675953897***
*MAKAMU MKUU WA SHULE-**0712869519.***
*PATRON-* ***0659 146804***
*TOVUTI:* ***www.samehighschool.wordpress.com***
***BARUA PEPE: sameboyshighschool@gmail.com.***

*Unapojibu tafadhali taja*
**Kumb.Na. SSS/K.16/KT/VOL.I/28.**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..........................
S.L.P.....................................
............................................

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SAME, HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME, MKOA WA KILIMANJARO, MWAKA 2022/2023.

### 1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika Shule hii kwenye tahasusi ya............ mwaka 2022/2023. Shule ya Sekondari Same ipo umbali wa kilometa 2.5 kutoka kituo kikubwa cha mabasi cha Same mjini, upande wa magharibi. Usafiri toka kituo cha mabasi cha Same mjini mpaka shuleni ni aidha pikipiki au Taxi. Nauli ya pikipiki ni Tshs. 1,000/= na ile ya Taxi ni Tshs. 4,000/=.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ................. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ...................... Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe...................

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### 2.1 SARE ZA SHULE.

Mwanafunzi anatakiwa kuja na **sare ya darasani** (ambayo ni suruali, shati, viatu, mkanda na soksi), **sare ya michezo** (ambayo ni track suit na raba), pia **sare nyinginezo** ambazo ni sweta na T-shirt.

#### 2.1.1 Sare ya Darasani:-

(i) Suruali mbili za rangi ya "**DARK BLUE**", aina ya Tetron. Mshono wa suruali uwe kama ifuatavyo:-

a) Upana wa chini inchi 17 na iwe na "turn-up".

b) Suruali iwe na "marinda"

Kipande cha kitambaa na picha ya mshono vimeambatanishwa kwa ajili ya rejea.

Aidha kwa maeneo ya huku same mjini suruali moja inapatikana kwa Tsh. 20,000/=. Hivyo kwa anayependa kushonea huku awe na fedha yake mkononi.

(ii) Shati mbili nyeupe za mikono mifupi aina ya tetron.

(iii) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, jozi mbili.

(iv) Mkanda mweusi wa ngozi wenye bakoli ya kawaida.

(v) Soksi za rangi nyeusi au Dark Blue, jozi mbili.

#### 2.1.2 Sare za Michezo

(i) Track suit ya rangi ya Blue. Kwa wale watakaohitaji kununulia huku Same mjini, inapatikana kwa Tsh. 25,000/=.

(ii) Raba za michezo za rangi yoyote, jozi moja.

#### 2.1.3 Sare Nyinginezo

(i) Sweta la rangi ya Dark Blue kwa ajili ya kujikinga na baridi. Kwa wale watakaohitaji kununulia huku Same mjini, linapatikana kwa Tsh. 15,000/=.

(ii) T-shirt mbili zenye "Collar" za rangi ya njano ambazo zitawekwa nembo ya shule kwa gharama ya Tsh.4,500/= kwa

kila moja. Kwa atakayependa kununulia shuleni, T-shirt yenye nembo ya shule inapatikana kwa Tsh. 15,000/= kila moja.

(iii) Suruali mbili za kitambaa cha rangi nyeusi (shamba dress) za heshima zitakazovaliwa baada ya muda wa vipindi vya darasani. Aidha kwa maeneo ya huku same mjini suruali moja inapatikana kwa Tsh. 20,000/=. Hivyo kwa anayependa kushonea huku awe na fedha yake mkononi.

- **Tanbihi:-** Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa mavazi mengine yoyote zaidi ya sare rasmi za shule kipindi chote awapo shuleni .
- Iwapo mzazi/ mlezi hatakuwa na uelewa mzuri wa vipimo na rangi za sare, ni vyema akashonea huku Same mjini kwa usimamizi wa karibu wa shule.

**2.2 MALAZI.**

(i) Godoro size ya $2^{1}/_{2}{}' \times 6'$.

(ii) Shuka mbili za rangi ya pinki.

(iii) Chandarua chenye sura ya umbo mraba,yaani "square".

(iv) Mto na foronya, zote ziwe za rangi ya pinki.

**2.3 VIFAA VYA USAFI**

(i) Ndoo moja na fagio la nje aina ya chelewa lenye mpini wa mti kwa matumizi binafsi ya usafi wa mwanafunzi.

(ii) ***"Jembe"*** moja na "***Hard-broom"*** moja kwa wanafunzi wa Tahasusi ya **PCM.**

(iii) Fagio la ndani moja aina ya ***"soft broom"*** na fagio moja la ndani aina ya ***"rubber squizer"*** kwa mwanafunzi wa Tahasusi ya **PCB.**

(iv) ***"Fyekeo***" (kwanja) moja na "***jembe***" moja kwa mwanafunzi wa Tahasusi ya **HGK, HGL na HKL.**

(v) Fagio la ndani moja aina ya ***"soft broom"*** na fagio la ndani moja aina ya ***"ruber squeezer"*** kwa mwanafunzi wa Tahasusi ya **CBG.**

**2.4 VIFAA VYA KITAALUMA**

**(i)** Faili mbili (folder file) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi.

**(ii)** Ream moja ya karatasi aina ya A4 kwa mwaka.

**(iii)** Scientific calculator kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi.

**(iv)** Daftari (Counter Books) za kutosha kulingana na masomo ya mwanafunzi.

**(v)** Vitabu vya masomo ya Tahasusi husika ambavyo ni mali ya mwanafunzi mwenyewe.

**(vi)** Result slip ya kidato cha nne

**(vii)** Cheti cha kuzaliwa (birth certificate).

## 2.5 MAHITAJI MENGINE MUHIMU

(i) Vyombo vya kulia chakula, e.g Sahani, Kikombe, Bakuli na Kijiko.

(ii) Sanduku imara la bati kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake.

(iii) Fedha ya matumizi binafsi (Pocket Money).

## 2.6 MICHANGO YA SHULE INAYOTAKIWA KULIPWA NA KILA MZAZI/MLEZI KWA MWAKA.

(i) Ada ya shule kwa mwaka Tshs 70,000/- (Unaweza kulipa Tshs 35,000/- kwa mhula)

| | |
|---|---|
| (ii) Mchango wa Taaluma | Tshs 20,000/- |
| (iii) Tahadhari (haitarejeshwa) | Tshs 5,000/- |
| (iv) Ukarabati wa Samani | Tshs 15,000/- |
| (v) Malipo kwa Wapishi, Walinzi na Vibarua wengine | Tshs 30,000/- |
| (vi) Kitambulisho na picha | Tshs 6,000/- |
| (vii) Nembo ya shule kwa ajili ya shati mbili | Tshs 3,000/- |
| (viii) Huduma ya kwanza | Tshs 10,000/- |
| (ix) Bima ya afya(CHF) | Tshs 5,000/- |
| Jumla | **Tshs 164,000/-** |

**Tanbihi:-** Jumla ya fedha ya ada na michango mingine yote hapo juu ni Tshs 164,000/=. Fedha yote hiyo iwekwe katika Benki ya NMB kwenye akaunti ya shule ijulikanayo kwa jina la **SAME SECONDARY SCHOOL, A/C No. 40501100002.** Bank pay – in – slip iliyoandikwa jina la mwanafunzi iwasilishwe shuleni kwa ajili ya kuandikiwa risiti.

## 3.0 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro.
(iii) Kugoma adhabu na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
(vi) Kufuga ndevu.
(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(viii) Uvutaji wa sigara.
(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja , kuoa au kuolewa.
(x) Kusababisha mimba kwa mwanafunzi au msichana mwingine yoyote.
(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xii) Kwenda kwenye majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xiv) Kudharau Bendera ya Taifa.
(xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, kuua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xvi) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

## 4.0 VITAMBULISHO NA FOMU MUHIMU.

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form), **Fomu "A"** iliyoambatanishwa ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara Mwanafunzi anaporipoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika Migomo, Fujo na Makosa ya jinai na;

c) Fomu ya Mzazi / Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Fomu ya Sehemu **(b)** na **(c)** hapo juu zimejumuishwa katika **Fomu "B"** iliyoambatanishwa. Hali kadhalika, **Fomu "B"** ikabidhiwe kwa Mkuu wa Shule mara mwanafunzi anaporipoti shuleni.

**d)** Picha 4 za wazazi/walezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi pamoja na namba zao za simu.

## 5.0 MWISHO

- Mwanafunzi na mzazi/mlezi anatakiwa kusoma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Zaidi ya hapo, mwanafunzi anapaswa kutumia akili au ufahamu wa kawaida, yaani "**COMMON SENSE**" katika kufanya maamuzi.

***KARIBU SANA SAME SEKONDARI.***

........................................................

**HOZA E. MGONJA**
**MKUU WA SHULE.**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI SAME

**FOMU A**

Shule ya Sekondari Same,
S.L.P 17,
**SAME**

Tarehe ....................

Kumb. Na. SSS/K.16/KT/VOL.I/20
Mganga Mkuu (Hospitali ya Serikali)

**YAH: MAOMBI YA KUMPIMA AFYA MWANAFUNZI**
**(JINA) ..........................................................................**

Mwanafunzi mtajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Same, kidato cha tano kwa mwaka wa masomo wa 2021/ 2022. Naomba apimwe afya yake, hasa kwa kuzingatia magonjwa yaliyoorodheshwa hapa chini. Weka alama ya vema (√) panapohusika.

1. Kifafa (Epilepsy) Ndiyo ....................Hapana.....................
2. Ugonjwa wa moyo (Heart Disease) Ndiyo .................. Hapana ..................
3. Magonjwa ya akili (Mental Illiness) Ndiyo .....................Hapana....................
4. Kifua kikuu (T.B) Ndiyo .....................Hapana ...................
5. Pumu (Asthma) Ndiyo .....................Hapana ...................
6. Kisukari (Diabetes) Ndiyo .....................Hapana ...................
7. Vidonda vya tumbo (Abdomianal Ulcers) Ndiyo .................... Hapana ...................
8. Kichocho (Bilharziasis) Ndiyo .......................Hapana ..................
9. Malaria sugu (Chronic Malaria) Ndiyo .......................Hapana ..................
10. Magonjwa ya zinaa (Venereal Diseases) Ndiyo ..................... Hapana ..................
11. Covid-19 Ndiyo.....................Hapana....................

    N.B. mwanafunzi atakayegundulika kuwa na ugonjwa wa covid-19 haruhusiwi kuripoti shuleni ,abaki nyumbani mpaka atakapothibitishwa kupona.
12. Magonjwa mengine (Yataje) ..........................................................................................
    ..........................................................................................................................

Jina la Mganga ..............................................................Sahihi ........................................

**Muhuri wa Ofisi ........................................**

Iwapo Mwanafunzi anaumwa, naomba atibiwe kabla ya kuripoti shuleni.

Ahsante.

..........................................
**H.E. MGONJA**
**MKUU WA SHULE.**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI SAME

## FOMU B

Shule ya Sekondari Same,
S.L.P 17,
**SAME**
**Tarehe..............................**

**KIAPO CHA KUTII KANUNI/ SHERIA ZA SHULE NA TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI.**

**SEHEMU YA MWANAFUNZI**

Mimi .......................................ninakiri na kuahidi kuwa nitatii sheria na kanuni za shule. Iwapo nitakiuka, hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa kadri inavyostahili. Pia naahidi kuwa nitawajibika vema katika Masomo Darasani na Kazi zote nitakazopangiwa Shuleni kwa utii wa hali ya juu na Mungu anisaidie.

Sahihi ya Mwanafunzi ..................................................................Tarehe ...............................

**SEHEMU YA MZAZI/ MLEZI**

Mimi ...........................................................................ambaye ni Mzazi / Mlezi wa .......................................................(Jina la Mwanafunzi) nakiri na kuahidi kuwa nitatoa ushirikiano mzuri kwa Uongozi wa Shule katika kumlea Kijana wangu. Hii ikiwa ni pamoja na kumlipia michango yote ya shule kwa wakati. Nitakuwa tayari kushirikiana na Uongozi wa shule katika suala zima la nidhamu ya Mwanafunzi na kwamba pale itakapolazimu kuitwa shuleni, kwa suala la Utovu wa nidhamu wa Mwanafunzi, nitakuwa tayari kuitika wito.

Sahihi ya Mzazi ..................................................................Tarehe ..................................

**TAARIFA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la Mwanafunzi ..................................................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa ..............................................................................
3. Taifa ..........................................................................................................
4. Mkoa ..........................................................................................................
5. Wilaya .......................................................................................................
6. Tarafa ...................................................................................................
7. Kata ..........................................................................................................
8. Kijiji ..........................................................................................................
9. Jina la Mzazi/ Mlezi ...........................................................................
10. Anuani kamili ya Mzazi/ Mlezi ............................Namba yake ya Simu .......................
11. Taarifa ya kubaini Wanafunzi yatima. Weka alama ya vema (√) panapohusika.

    Baba na mama wote wamefariki ( )
    Baba yupo na mama alifariki ( )
    Mama yupo, na baba alifariki ( )

12. Jina la shule ya Sekondari aliyotoka ............................Wilaya shule hiyo ilipo ..............................
13. Kazi ya Mzazi/ Mlezi ...........................................................................................
14. Jina la Mzazi/ Mlezi mbadala (iwapo Mzazi/ Mlezi hatapatikana) .......................................................Anuani kamili ...................................Namba ya Simu ..........................